
# Mradi wa Uimarishaji wa Huduma Muhimu za Afya (MUHUMA)

*(Mradi wa pamoja kati ya Wizara ya Afya na Shirika la Kimataifa la Maendeleo na Utafiti la Canada (IDRC)*

## Muhtasari Na. 2: Jedwali linaloonyesha athari za magonjwa katika wilaya



*Mfumo wa Utoaji wa takwimu unaelezwa kuwa ni: Utoaji wa habari kulinagana na sehemu maalum ya jiografia na kuzifuatilia na hatimaye kutoa takwimu kuhusu kuzaliwa kwa watoto, uhamiaji na vifo.Habari hizi zinapatika kwenye mtando:* www.indepth-network.net



# *Ushahidi ulio wazi*

Mradi wa Uimarishaji wa Huduma Muhimu za Afya (MUHUMA) ni mradi wa pamoja kati ya Wizara ya Afya na Shirika la Kimataifa la Maendeleo na Utafiti la Canada (IDRC). Mradi unajishughulisha na tafiti ambazo kutokana na ushahidi wake zinaweza kuongoza katika uaandaji wa mipango ya afya. MUHUMA inalenga katika kuiarifu jamii kuhusu matokeo ya utafiti wake na mafunzo ambayo imeyapata pamoja na mbinu ambazo zimeonyesha mafanikio katika utekelezaji na tayari zimetumiwa katika wilaya ambazo ziko ndani ya mradi huu.

**Maelezo ya awali: Athari za magonjwa**

Mzigo wa athari za magonjwa ni jumla ya miaka inayopotea kutokana na kufa mapema na ulemavu. Katika Afrika, asilimia 80 ya athari za magonjwa inatokana na kufa mapema. Kwa sababu watu wengi wanakufa majumbani au nje ya vituo vya huduma ya afya, taarifa kutoka katika vituo vya tiba hazitoi picha halisi ya matatizo ya kiafya ambayo yanaikumba jamii. Zaidi ya hapo, usajili wa vizazi na vifo ni jambo ambalo ni nadra kufanyika katika nchi nyingi kusini mwa Jangwa la Sahara.
Katika hali hiyo, utaratibu wa kukusanya takwimu kwa njia ya sensa ya mara kwa mara katika ngazi ya kaya unaweza kuwasaidia wanajamii katika kudodosa habari na upatikanaji wa habari ambazo zinaweza kuonyesha ukubwa wa tatizo la magonjwa na vifo vinavyotokea vijijini.

Wakiwa na ushahidi kama huo, waandaaji wa mipango wanaweza kuchagua kugharamia huduma zenye tija zaidi. Kwa mfano, Mpango wa Tiba Mtoto (IMCI). Mpango huu unalenga kutibu magonjwa matano ya watoto chini ya miaka 5: malaria, kichomi, kuharisha, surua na utapiamlo. Katika wilaya ya Rufiji, Mfumo wa Kuweka Hesabu ya Watu kwa Kupitia Kaya hadi Kaya umeonyesha kwamba magonjwa haya matano yanachangia asili mia 34 ya mzigo wa athari za magonjwa.

**Tatizo ambalo linazungumziwa**

Takwimu ambazo zimekusanywa chini ya Mfumo wa Kuweka Hesabu ya Watu Kupitia Kaya hadi Kaya, bado hazijapata nafasi ya kupitiwa katika ngazi ya waandaji wa mipango ya maendeleo katika wilaya.

**Ufumbuzi:**

Jedwali la athari ya magonjwa linahusisha mawasiliano kwa kuziweka takwimu za athari ya magonjwa katika picha na michoro iliyoambatana na maelezo mafupi na rahisi kwa kila mchoro. Badala ya kuwasilisha athari za magonjwa kwa njia ya aina ya maradhi, chombo hiki huzingatia asilimia ya athari za magonjwa inayoshughulikiwa na aina moja ya huduma au mkakati.

Zile huduma ambazo zina tija zaidi na zinakabili zaidi ya asilimia mbili ya athari ya magonjwa ndiyo zinazojumuishwa kutengeneza kitata cha huduma zitakazochaguliwa na wanamipango wa wilaya. Aidha chombo hiki hutoa taarifa kuhusu mahali kilipotokea kifo na sehemu alikopata huduma mgonjwa kabla ya kifo.

## Chombo/zana hii inavyotumiwa:

Jedwali la athari ya magonjwa hutayarishwa kila mwaka ili liweze kutumika wakati wa kutayarisha mipango ya afya ya wilaya zilizopo katika mradi.
Kwa njia hiyo, Timu ya Afya ya Halmashauri ya Wilaya hugawa raslimali chache waliyokuwa nayo kutoa huduma zinazokabili sehemu kubwa ya athari za magonjwa. Zoezi hili hurahisishwa zaidi na zana/chombo kingine -District Health Account Tool (Muhtasari namba 3).
Mfumo wa kitaifa utakaotoa taarifa ya vifo na kuzaliwa katika ngazi ya kaya ndio hatimaye utakaohusika katika kutayarisha na kusambaza chombo/zana hii katika wilaya zote.

## Jedwali linaonyesha athari ya magonjwa ambayo yametolewa taarifa na jinsi linavyotumika.

Majedwali haya hutayarishwa kila mwaka na kuunganishwa katika mzunguko wa mpango ambao hutayarishwa na kuhusishwa katika wilaya ambazo ziko chini ya mradi huu.
Menejimenti za Afya katika Halmashauri za Wilaya hutumia majedwali haya kama hatua yao ya mwanzo ya kuweka vigezo kwa mtiririko wa umuhimu na hivyo kutoa mwongozo wa jinsi ya kupambana na magonjwa yanayowasumbua zaidi wananchi na kuyatafutia ufumbuzi.
Kwa njia hiyo, Menejimenti ya Afya katika Halmashauri ya Wilaya hutenga fedha na raslimali iliyopo ili kuweza kushughulikia magonjwa ambayo yamepewa kipaumbele katika mtiririko wa kuyashughulikia. Zoezi hili linarahisishwa zaidi na mkakati mwingine wa MUHUMA kwa kutumia Mfumo wa Bajeti ya Huduma za Afya katika Wilaya (Muhtasari Namba 3).

Mfumo wa Kitaifa utakaokusanya taarifa za kuzaliwa na vifo katika ngazi ya kaya kutoka katika wilaya zilizochaguliwa, ndio hatimaye, utahusika katika kutayarisha na kusambaza jedwali la athari za magonjwa.
Mfumo wa kuweka jedwali la hesabu za watu kupitia kaya hadi kaya unatoa taarifa zote ambazo zinahitajika katika huduma ya afya.


---

**Kutoka kwa watekelezaji wa huduma ya afya: Dr. Harun Machibya, Mganga Mkuu wa wilaya ya Morogoro Vijijini**

"Kabla ya kuanza kutumia mfumo huu, mipango yetu haikuonyesha ukweli uliopo katika uwanja wa huduma ya afya. Katibu wa Afya katika wilaya alikuwa akikaa chini na Mhasibu na kuongeza asilimia 10 - 20 kwa kulinganisha na bajeti ya mwaka uliotangulia. Kwa kweli, huu haukuwa mpango kwa maana ya mpango, bali ulikuwa ni kutengeneza bajeti tu. Kwa mfumo wa bajeti kama huo, tulizingatia na kutilia mkazo zaidi masuala ya utawala kuliko kuwa na kituo safi cha huduma ya afya."
"Kwa sasa chini ya mfumo huu mpya, tunaweza kupanga mipango yetu kwa uhakika zaidi na kuweka kipaumbele katika utoaji wa huduma za afya kwa sababu tunazo taarifa zote kuhusu magonjwa ambayo yanawasumbua zaidi wananchi kutoka kwao wenyewe."

Mahali pa kupata habari zaidi
Pata habari kutoka Jedwali linaloonyesha magonjwa kutoka TEHIP website:www.idrc.ca/tehip
Burden of Disease Profile 2000, Coastal Zone
Wasiliana na:
Mradi wa Uimarishaji wa Huduma Muhimu za Afya (MUHUMA),
Sanduku la posta 78487,
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: (255) (022) 213 0627,
Fax: (255) (022) 211 2068
Barua Pepe: admin@tehip.or.tz

---




**Burden of Disease Profile: Graph shows how much of the total burden of disease is addressed by each essential health intervention strategy currently available at district level.**